## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

### HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

### SHULE YA SEKONDARI WILLIAM LUKUVI


Mkuu wa Shule +255621420290/0764826936

godwinisaya0@gmail.com

Makamu Mkuu wa Shule+255621419616

Mwalimu wa Taaluma +255621426531

Shule ya Sekondari William Lukuvi

S.L.P 2599

**IRINGA.**


**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….……………………………………………..……......**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI WILLIAM LUKUVI HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**

***Simu ya mkononi/laini/kifaa chochote cha umeme ni adui wa Taaluma. Ni marufuku. Ukikamatwa utafukuzwa shule***

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2026 na atasoma tahasusi ya …………
Shule hii ya Sekondari William Lukuvi ipo umbali wa kilomita **hamsini na tatu (53)** kutoka Iringa mjini. Unaanzia stendi kuu ya mabasi Iringa (IGUMBILO) kwa wale wanaotokea barabara ya Morogoro-Dar es Salaam au Njombe -Mbeya utapanda daladala Kutoka igumbilo kwenda Iringa mjini (stedi ya daladala) na Kwa wale wanaotokea barabara ya Dodoma wata shuka stendi ndogo ya Kihesa Iringa mjini kisha watapanda bajaji kwenda stendi ya Daladala Iringa mjini. Kisha panda mabasi ya kutoka Iringa mjini kwenda Pawaga na utashuka kibao cha shule ya sekondari William Lukuvi. Nauli kutoka Iringa mjini hadi shuleni ni shilingi elfu sita (6000). (Mabasi ya kuja shule yanapatikana stendi ya Daladala Iringa mjini katikati ya Manispaa ya Iringa, Mabasi yanaanza safari zake kuanzia saa 5 asubuhi hadi saa 11 jioni kila siku)

Muhula wa kwanza wa Masomo unaanza tarehe **.............,** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **..................**

**1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**Sare za Shule**

(i) Suruali mbili za rangi ya dark blue (esteem 2) zenye malinda mawili, pindo (turn up) na zisizobana zenye upana wa si chini ya sentimita 17. (**asiyefuata maagizo haya hatapokelewa**)
(ii) Shati mbili nyeupe mikono mirefu zenye vifungo (vishikizo) aje nazo.
(iii) Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili vya kufunga kwa kamba. (**lizingatiwe)**.
(iv) Soksi jozi mbili rangi “**kijivu**”
(v) Sweta moja la muundo wa V rangi ya kaki (**Aidha Asiyepata**, anaweza kupata shuleni kwa shilingi **13,000**).
(vi) Aje na shilingi **13,000/=** kwaajiri ya T-shirt moja yenye kola (maarufu kama form six) kwaajiri ya sare maalumu ya darasani.
(vii) Mkanda mweusi (Jozi mbili), na usiwe mpana.
(viii) Kandambili jozi moja.
(ix) Aje na Tai mbili ndefu rangi ya dark bluu (**Aidha**, asiyepata anaweza kuzipata shuleni kwa shilingi **3,000 kwa kila tai).**

**NB.zingatia vizuri rangi za Sare za shule ili kuepuka gharama zisizo za lazima angalia kiambatanisho A, ukurasa wa mwisho.**

**Sare za kushindia (After classes dress)**

(i) Suruali mbili za kitambaa rangi kijani jeshi zenye mkunjo (turn up) zisizo za kubana,upana si chini ya 17cm.

(ii) Track suit moja rangi ya kijani jeshi.

(iii) T¯shirt 2 rangi ya njano (round kola plain /isiyo na maandishi wala alama yoyote)

(iv) Viatu vya kushindia –Raba nyeusi za kufunga na Kamba

**Sare za Michezo**

(i) raba/viatu rangi yoyote,

(ii) Bukta,Tshirt (fulana) na soks ndefu **vyote Jezi ya TAIFA STARS YA RANGI YA BLUU.** Kwa ajili ya michezo (**vitakaguliwa)**

**NB. Mwanafunzi hataruhusiwa kuwa na mavazi mengine zaidi ya haya yaliyoelekezwa.**

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

(i) Godoro lenye upana wa futi 2.5(Godoro anaweza kulipata pia katika maduka yaliyopo karibu na maeneo ya shule), Mto na foronya na Chandarua

(ii) Aje na Blanketi Jepesi moja,Shuka mbili za rangi ya Pinki,.

(iii) Sabuni za kufulia na kuogea za kutosha, Mswaki na dawa ya meno.

(iv) Sanduku moja imara la kutunzia vitu vyake.(tranka)

(v) Aje na kidumu cha lita tano kwa ajili ya kuwekea maji ya kunywa

(vi) Aje na vyombo vya chakula(vinapatikana kwenye duka la shule) .

(vii) Aje na tochi/taa ya betri **"*isiwe ya kuchaji kwa kutumia umeme*"**.

**Vifaa vya Taaluma**

(i) Counterbook 10 (3 quires)

(ii) Madaftari ya msomi (dozen moja)

***Simu ya mkononi/laini/kifaa chochote cha umeme ni adui wa Taaluma. Ni marufuku. Ukikamatwa utafukuzwa shule***

(iii) Kalamu za wino rangi ya blue au njeusi box moja

(iv) Penseli na ufuto wake dosen moja

(v) Mathematical set moja(**lazima**)

(vi) Scientific calculator(**lazima**)

(vii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa mchepuo wa **CBG**-Lazima

(viii) Koti la Maabara rangi nyeupe moja mikono mirefu kwa wanafunzi wa **CBG** ni **Lazima**.

(ix) Buti ndogo za wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi (**Lazima)**

(x) Graph Pad Mbili kwa kila mwanafunzi(**Lazima**)

(xi) Rimu moja kwa muhula ya karatasi za A4 (**lazima)**

(xii) Saa ya mkononi kwa kila mwanafunzi kwa matumizi binafsi (**Lazima**):

Mzazi anashauriwa kumnunulia mwanae vitabu vya kiada na ziada,
**NB. Orodha ya vitabu vya masomo husika**

**Vifaa vya Usafi na Mazingira**

**Kila mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi shuleni;**

- Soft bloom moja
- Squizer moja
- Hard bloom moja
- Mfagio wa chelewa mmoja
- Jembe lenye mpini.
- Ndoo kubwa moja (lita 20) na ndogo moja (lita 10)

**1.1 Michango mbalimbali ilipwe kwenye akaunti ya shule NMB 60501100117 jina WILLIAM LUKUVI SECONDARY SCHOOL**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Kitambulisho | 5,000/= |

***Simu ya mkononi/laini/kifaa chochote cha umeme ni adui wa Taaluma. Ni marufuku. Ukikamatwa utafukuzwa shule***

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Nembo | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya OWR – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**GODWIN CHARLES ISAYA**
**MKUU WA SHULE**
**godwinisaya0@gmail.com**
**SHULE YA SEKONDARI WILLIAM LUKUVI**

# <u>MUHIMU SANA</u>

**NI LAZIMA KILA MWANAFUNZI AJE NA KADI YAKE YA BIMA YA AFYA KWAAJILI YA MATIBABU. AIDHA KAMA MWANAFUNZI HANA KADI HIYO UNATAKIWA KUMPA MWANAO FEDHA (TSHS 50,400) KWAAJILI YA KUMTENGENEZEA KADI HIYO. MWANAFUNZI ASIYE NA BIMA YA AFYA HATAPOKELEWA SHULENI. MZAZI/MLEZI ZINGATIA AGIZO HILI ILI KUEPUKA USUMBUFU UNAOWEZA KUJITOKEZA.**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule +255621420290/+255764826936**
- **Makamu Mkuu wa Shule +2555621419616**
- **Mwandamizi Taaluma +255621426531**

**SEHEMU; D, Fomu Na2 -B**

**TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI**

Shule inapenda kupata taarifa muhimu za kila mwanafunzi kwa ajili ya mawasiliano wakati wote awapo shuleni. **Fomu hii ijazwe kwa usahihi na ukamilifu**.

Jina la mwanafunzi …………………………………… Kidato…………. mchepuo................... Mwaka…………

Anwani ya nyumbani (anayotumia)………………………………Tarehe ya kuzaliwa…………………

Kama ni mlemavu, aina ya ulemavu…………………………………taarifa za wazazi, mzazi moja……………… wazazi wawili………………..yatima ……………..

Namba ya simu(ya nyumbani/ya mzazi)……………………Mtaa/Kijiji anachotoka…………………..Kata……………. Tarafa………………...Wilaya………………Mkoa…………………..shule ya msingi aliyosoma……………….

Shule ya Sekondari atokayo……………………… Namba ya Mtihani ya Kidato cha Nne……………

Anwani ya shule ………………………Matokeo yake ya kidato cha nne………………………………

Dini yakeni …………………[Mkristo, Mwislamu n.k.] Dhehebu lakeni……………… Mkatoliki, Mlutheri,Suni n.k}

Sahihi ………………………………… Tarehe……………………………...

**NB. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili Dini akiwa shuleni.**

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi……………………………………….. NAKUBALI / SIKUBALI nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari William Lukuvi. Naahidi kuwa nitazitii taratibu, kanuni na sheria zote za shule. Nitafuata masharti yote yanayotolewa na Mkuu wa shule, Wafanyakazi wote na Viongozi wote wa shule. Ninaahidi pia nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo kwa muda wote nitakaokaa William Lukuvi Sekondari. Nakiri kuwa kwa akili zangu timamu, taarifa zote nilizotoa hapo juu ni sahihi na zinanihusu.

Jina ……………………………………….. sahihi ………………………Tarehe ………………..…

**TAARIFA YA MZAZI/ MLEZI**

Jina la Mzazi/ Mlezi ……………………………………………………………………….

Anwani yake………………………………………………………………………………

Namba ya simu ……………………………………………………………………………..

Kazi anayofanya……………………………………………………………………………

Wilaya/Mji anakofanyia kazi………………………………………………………………

Anwani ya kazini…………………………………………………………………………..

Namba ya simu ya kazini ……………………………………………………………….............

***Simu ya mkononi/laini/kifaa chochote cha umeme ni adui wa Taaluma. Ni marufuku. Ukikamatwa utafukuzwa shule***

## AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi……………………………………..MZAZI/MLEZI NAKUBALI / SIKUBALI nafasi aliyopewa mwanangu katika shule ya sekondari William Lukuvi. Naahidi kuwa nitawajibika/sitawajibikana kumhimiza mwanangu kuzitii taratibu, kanuni na sheria zote za shule. Nitashiriki/sitashiriki kumhimiza kufuata masharti yote yanayotolewa na Mkuu wa shule, Wafanyakazi wote na Viongozi wote wa shule. Ninaahidi pia nitashirikiana/sitashirikiana na uongozi wa shule kumhimiza mwanangu kushirikiana na wanafunzi wenzake katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo na kuwa na nidhamu kwa muda wote atakaokaa William Lukuvi Sekondari. Nitapenda/sitapenda kupata taarifa zote zinazomhusu mwanangu muda wote awapo shuleni***(futa isiyohusika)***

**Jina la mzazi/mlezi……………………………………..Sahihi…………………………Tarehe……………………….**

**WATU WA KARIBU(KIUHUSIANO/UNDUGU) NA FAMILIA AMBAO UNGEPENDA WAPATE TAARIFA ZAKO ZAIDI YA WAZAZI/ WALEZI**

(i) Jina………………………………………………… Anwani ……………………………………

Namba ya simu……………………………… Kazi anayofanya ……………….…………………

Uhusiano wake na mwanafunzi…………………………………..........................................................

(ii) Jina **…………………………………………………** Anwani …………………………………….

Namba ya simu……………………………… Kazi anayofanya ……………….……..……………

Uhusiano wake na mwanafunzi…………………………………..........................................................

(iii) Jina **……………………………………………………….**Anwani ……………………………………

Namba ya simu……………………………… Kazi anayofanya ……………….…………………

Uhusiano wake na mwanafunzi…………………………………......................................................

***NB; Iwapo anwani ya mmojawapo wa Mzazi/Mlezi au ndugu wa karibu amehama au Amefariki lazima mwanafunzi atoe taarifa na kubadilisha jina na kuandika mtu mwingine ambaye atawajibika kwa mwanafunzi***

**SEHEM; E, Fomu Na 3- C**

**FOMU HII IJAZWE NA MGANGA MKUU WA MKOA /WILAYA NA MWANAFUNZI AJE NAYO SHULENI NA KUIKABIDHI KWA MKUU WA SHULE.**

Mimi (Jina la Mganga Mkuu wa Mkoa/Wilaya) ………………………………………………..

Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi)………………………………..

Amepimwa na mimi kikamilifu na kuonekana kuwa anayo /hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo;

**(A) Hali ya Mwili.**

- (i) Mapigo ya moyo…………………………………………………………
- (ii) Damu (Haemoglobin)…………………………………………………..…..
- (iii) Kundi la Damu (Blood group) ……………………………….……………...
- (iv) Mkojo……………………………………………………………………
- (v) Haja kubwa………………………………………………………………
- (vi) Macho …………………………………………………………………
- (vii) Masikio ……………………………………………………………..

NB. Weka maoni yako kuhusu kile kilichotajwa…………………………………..

…………………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………….

**(B) Magonjwa.**

Amewahi /hajawahi au hana magonjwa yafuatayo;

- (a) Kifua kikuu (TB)…………………………………………………….…
- (b) Kifafa (Epilepsy)………………………………………………………
- (c) Shinikizo la damu (BP)…………………………………………………..
- (d) Magonjwa ya tumbo ……………………………………………………..
- (e) Seli mundu (Sickle cells) …………………………………………….……
- (f) Ukoma……………………………………………………………………
- (g) Magonjwa ya zinaa (taja aina) ………………………………………………
- (h) Ugonjwa wa akili ……………………………………………………..…
- (i) Ugonjwa mwingine nje ya orodha hapo juu ….…………………………….. ………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………..

**Maoni ya Daktari** ……………………………….……………………………………

………………………………………………………………………………

Saini na Muhuri wa Daktari/Mganga wa Hospitali ya Serikali.

***Simu ya mkononi/laini/kifaa chochote cha umeme ni adui wa Taaluma. Ni marufuku. Ukikamatwa utafukuzwa shule***

**SEHEMU;F,Fomu na4- D**

**ORODHA YA VITABU VYA MASOMO (mzazi/mlezi unaweza ukamnunulia mwanao)**

**CHEMISTRY**

**1.**Physical chemistry, by Delungu (Mzumbe bookshop project 1998)

2. Advanced inorganic chemistry part I and II(Tanzania institute of education).

3.Organic Chemistry part 1, The fundamental principles I.L finar (longman LTD)

4. Conceptual Chemistry for class XI-Chand

5.Conceptual Chemistry for class XII-Chand

**GEOGRAPHY**

1.Principles of physical geography by F J monk house

2. Geography integrated approach by D.waugh

3.Fundamental of Practical Geography by Josephat Mwita

4.General geography in diagram by R B burnet

5. Simplified physical Geography(A-LEVEL) by D M

6. Statistical methods and the geographers by s. Gregory

**7.Practical geography For Advanced secondary schools by TIE**

**BIOLOGY**

1.Biological science;Cambridge university press 1997 3rd edition

2.functional approach by Mbv Robert

3.New Understanding Biology By Suzan Toole

4. Advance biology Principles and application By C J Clegg and Mackean

5.Advanced Biology By Michael kent (2000).Oxford university press uk.

**BASIC APPLIED MATHEMATICS**

Basic applied Mathematics by Kiza and Septine I sillem

**HISTORY**

1.Advanced learners, History form V and six (history 1 and 2)( oxford 2011)

2.Advanced level History for Africa, From Neolithic Revolution to present (zist Kamili 2010)

3. Major events in the world History

4. Advanced level History (Nyambari nyangwine 2007

***Simu ya mkononi/laini/kifaa chochote cha umeme ni adui wa Taaluma. Ni marufuku. Ukikamatwa utafukuzwa shule***

5.Focus on Modern world history by Japhace, Ponsian, Chakupewa, Mpandije Yusuph P Maunda (2012)

**ENGLISH LANGUAGE**

1. Oxford Learners Dictionary
2. Advanced Level Literature By Nyambari Nyangwine
3. Advanced Level English Language one Form 5 & 6 By Shadrack Ndambo ana James Kinunda.

**KISWAHILI**

1. Kiswahili 1
2. Kiswahili 2
3. Tahakiki ya kidato cha 5&6 by Nyambari Nyangwine
4. Nadharia ya Lugha by Nyambari Nyangwine

**Kiambatanisho A**

# RANGI ZA SARE ZA SHULE

1. RANGI YA SURUALI YA DARASANI (DARK BLUU)



***Simu ya mkononi/laini/kifaa chochote cha umeme ni adui wa Taaluma. Ni marufuku. Ukikamatwa utafukuzwa shule***

2. T-SHIRT YA KUSHINDIA (RANGI YA NJANO PLAIN ROUND KOLA



3. RANGI YA KITAMBAA CHA SURUALI YA KUSHINDIA (KIJANI JESHI)



***Simu ya mkononi/laini/kifaa chochote cha umeme ni adui wa Taaluma. Ni marufuku. Ukikamatwa utafukuzwa shule***

4. RANGI YA TRUCK SUIT (KIJANI JSHI)



5. RANGI YA SWETA (RANGI YA KAKI)



*Simu ya mkononi/laini/kifaa chochote cha umeme ni adui wa Taaluma. Ni marufuku. Ukikamatwa utafukuzwa shule*

6. KOTI LA MAABARA KWA WANAFUNZI WA CBG



***Simu ya mkononi/laini/kifaa chochote cha umeme ni adui wa Taaluma. Ni marufuku. Ukikamatwa utafukuzwa shule***